14. Kazi za Kamati ya Mkoa.
15. Kamati za Wilaya.
16. Kazi za Kamati za Wilaya.
17. Mamlaka ya Kamati za Mikoa na Wilaya.
18. Kamati za Kata.
19. Kazi za Kamati za Kata.
20. Kamati za vijiji.
21. Kazi za Kamati za vijiji.
22. Utoaji wa taarifa za shughuli za usimamizi wa maafa
23. Miongozo ya kamati za maafa.
24. Kanuni za shughuli za kamati za maafa.

SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA KULINDA RAIA

25. Utaratibu wa kulinda raia.
26. Wajibu wa jumla.

SEHEMU YA TANO
OPARESHENI WAKATI WA MAAFA NA HALI YA HATARI

27. Kutangaza eneo la maafa.
28. Hali ya dharura inayopelekea kusababisha maafa.

SEHEMU YA SITA
MPANGO WA TAIFA WA USIMAMIZI WA MAAFA

29. Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.

SEHEMU YA SABA
MFUKO WA USIMAMIZI WA MAAFA

30. Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.
31. Usimamizi wa michango na misaada.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

32. Vyanzo vya fedha
33. Taarifa ya mwaka ya mahesabu.
34. Uwasilishaji wa taarifa ya mwaka.
35. Usimamizi na udhibiti wa fedha.
36. Bajeti ya mwaka na ya nyongeza.
37. Kanuni za uendeshaji.
38. Uwezo wa kuwekeza.

SEHEMU YA TISA
MAKOSA NA ADHABU

- 39. Makosa na adhabu.
- 40. Makosa yanayofanyika na kampuni.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MENGINEYO

- 41. Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa.
- 42. Kinga dhidi ya mashtaka.
- 43. Kanuni.
- 44. Kufuta na kubakiza Sura.

—
JEDWALI
—

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA.7 YA 2015

NAKUBALI,

JAKAYA MRISHO KIKWETE

Rais

11 Mei, 2015

Sheria kwa ajili ya kuanzishwa kwa Wakala wa Usimamizi wa Maafa; usimamizi wa athari za maafa; mfumo wa uratibu wa kuzuia maafa, kupunguza maafa, utayari, muitikio na uokoaji na usimamizi wa Mfuko wa Usimamizi wa Maafa na mambo kuhusiana na hayo.

[.....]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA

MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe
ya kuanza
kutumika

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka, 2015 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kupitia Tanguzo la Serikali litakalochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*.

Matumizi
Tafsiri

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

3. Katika sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

“Wakala” maana yake ni Wakala wa Usimamizi wa Maafa Tanzania unaoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

“afisa muidhiniwa” maana yake ni mtu yeyote aliyeidhinishwa kutekeleza shughuli yeyote kama atakavyoelekezwa na Wakala;

- “Baraza” maana yake ni Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania linaloanzishwa chini ya kifungu cha 7;
- “Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala anayeteuliwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;
- “maafa” maana yake ni tukio au mfululizo wa matukio, ama ya asili au yanayosababishwa na shughuli za binadamu, yanayosababisha au kutishia kuathiri ama kuharibu mfumo wa jamii, na kusababisha madhara ya kibinadamu, kiuchumi au mazingira ambayo jamii iliyoathirika haiwezi kukabili kwa kutumia rasilimali zake;
- “eneo la maafa” maana yake ni eneo lililotangazwa kuwa eneo la maafa chini ya Sheria hii;
- “Usimamizi wa maafa” maana yake ni mchakato endelevu unaoshirikishi sekta mbalimbali katika kupanga na kutekelezaji mikakati inayolenga-
- (a) kuzuia hatari au tishio la maafa;
 - (b) kupunguza kiwango cha athari au matokeo ya maafa;
 - (c) kuanzisha au kuimarisha juhudi za kujiandaa dhidi ya maafa;
 - (d) kuanzisha njia za haraka na ufanisi za kukabiliana na maafa;
 - (e) kuanzisha au kuimarisha njia za kurejesha hali baada ya maafa.
- “kujiandaa na maafa” maana yake ni hali ya kuwa tayari kukabiliana na tishio la hali ya maafa, maafa na athari zake;
- “uzuiaji wa maafa” maana yake ni hatua zinazochukuliwa kuondoa au kuzuia matukio ya kibinadamu au ya asili yasisababishe kutokea kwa maafa;
- “kurejesha hali baada ya maafa” maana yake ni hatua zinazosaidia kurejesha hali ya mfumo wa maisha, mali na kiwango cha uzalishaji cha jamii zilizoathirika, kurejesha miundombinu muhimu, uwezo wa uzalishaji, taasisi na huduma zilizoharibiwa au kuonekana kutokufanya kazi kutokana na maafa na kusaidia kuleta maendeleo endelevu kwa kufanya marekebisho muhimu kwa mabadiliko yaliyosababishwa na maafa au kuboresha na kurudisha katika hali ya kawaida;
- “kukabiliana na maafa” maana yake ni hatua yoyote inayochukuliwa muda mfupi kabla au mara tu baada ya maafa inayochukuliwa kuokoa maisha, kulinda mali na mazingira au kushughulikia uharibifu uliotokea na madhara mengine yaliyosababishwa na maafa;

- “upunguzaji wa athari za maafa” maana yake ni hatua zinazochukuliwa kupunguza uwezekano wa matokeo yenye athari ya maafa kama vile vifo, majeruhi, uwezekano wa upotevu wa mali, mfumo wa maisha, kuathirika kwa shughuli za kiuchumi au uharibifu wa mazingira unaotokana na mwingiliano wa majanga ya asili au ya kibinadamu na mazingira hatarishi;
- “Kamati ya Wilaya” maana yake ni Kamati ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;
- “hatarishi” maana yake ni hali ya tukio la hatari, kitu au shughuli ya kibinadamu au hali ambayo inaweza kusababisha upotevu wa maisha, athari au madhara ya kiafya, uharibifu wa mali, upotevu wa riziki za maisha ya watu na huduma, na uharibifu wa kijamii na kiuchumi;
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Usimamizi wa maafa;
- “kupunguza” maana yake ni hatua zinazoelekezwa kupunguza athari au madhara ya maafa;
- “Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa” maana yake ni mpango ambao unaelezea hatua zitakazochukuliwa katika kushughulikia maafa, kupunguza hatari na Usimamizi wa maafa;
- “maafa ya asilia” maana yake ni maafa yanayotokana na mwingiliano wa matukio ya asili bila kusababishwa na binadamu na inajumuisha matukio kama vile, tetemeko, kimbunga, mafuriko, ukame, moto au magonjwa ya mlipuko;
- “Jukwaa” maana yake ni Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa lililoanzishwa chini ya Sheria hii;
- “Kamati ya Mkoa” maana yake ni Kamati ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;
- “Kamati ya Kijiji” maana yake Kamati ya Kijiji ya Usimamizi wa Maafa iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;
- “uwezekano wa kuathirika” maana yake ni kiwango cha uwezekano wa watu kupatwa au kuathirika na maafa.
- “Kamati ya Kata” maana yake ni Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya Kata iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;

SEHEMU YA PILI

WAKALA WA USIMAMIZI WA MAAFA

4.-(1) Unaanzishwa wakala ambao utajulikana kama Wakala wa Usimamizi wa Maafa Tanzania.

(2) Wakala utakuwa ni kampuni hodhi, na kwa jina lake hodhi utakuwa na uwezo wa-

- (a) kushtaki na kushtakiwa;
- (b) kuingia katika mikataba, makubaliano, waraka wa makubaliano, hati na kutekeleza mipangilio mingine;
- (c) kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika; na
- (d) kuwa na muhuri wake.

(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa na haki ya kuingilia kati shauri lolote au jambo lolote lililofunguliwa na au dhidi ya Wakala.

Sura ya 5

(4) Endapo, Mwanasheria Mkuu ataingilia kati shauri lolote, masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali yatumika, katika shauri au jambo hilo kama kwamba yamefunguliwa na au dhidi ya Serikali.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu cha (3) na (4), Wakala utakuwa na wajibu wa kumfahamisha Mwanasheria Mkuu kuhusu shauri lolote ambalo liko mahakamani au kusudio la kufungua shauri au kupeleka suala kwa au dhidi ya Wakala.

Kazi za
Wakala

5.-(1) Wakala utakuwa ni kitovu cha taifa cha kuratibu upunguzaji wa hatari na Usimamizi wa maafa.

(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu masharti ya kifungu kidogo cha (1), Wakala-

- (a) utaandaa sera na mipango kuhusu shughuli zote zinazohusiana na usimamizi wa maafa Tanzania Bara;
- (b) utakuwa kituo kikuu cha kupanga, taasisi ya uratibu na ufuatiliaji katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa, kukabilia na kurejesha hali kwa kuzingatia hatari zote za maafa zinazoweza kujitokeza;
- (c) utaratibu na kufuatilia wizara, sekta mbalimbali na kamati za kitaalam zenye dhamana ya Usimamizi wa maafa katika ngazi zote;
- (d) utaunda Kituo cha Dharura cha Usimamizi wa Maafa;
- (e) utaunda mfumo wa tahadhari ya awali utakaojumuisha sekta zote na kuwa kiungo kati ya asasi mbalimbali zinatoa huduma ya tahadhari;
- (f) utaendeleza elimu, maarifa na utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano katika Usimamizi wa maafa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma;

- (g) kutafuta rasilimali kwa ajili ya Usimamizi wa shughuli za maafa; na
- (h) kuhitaji kutoka taasisi yoyote, idara, mamlaka, mtu au watu, kuwasilisha taarifa inayohitajika kwa ajili ya shughuli za Usimamizi wa maafa kama Mkurugenzi atakavyoelekeza.

Mamlaka ya
wakala

6.-(1) Kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake, Wakala utakuwa na mamlaka ya-

- (a) kuamuru watu kuondoka katika meneo ya maafa au maeneo hatarishi;
- (b) kusimamisha au kuzuia uuzaji wa vileo, vinywaji, silaha, milipuko, au vitu vingine ambayo vitaonekana havipaswi kuwa kwenye maeneo ya maafa; na
- (c) kuchukua na kutumia rasilimali za Serikali ikijumuisha maghala, vifaa na nyenzo nyingine kama itaonekana ni muhimu kwa shughuli za dharura.

(2) Wakala utatekeleza mamlaka yanayohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa maelekezo yoyote yaliyotolewa chini ya mamlaka yake na kuchukua au kusababisha kuchukuliwa kwa hatua hizo ikijumuisha kupeleka shauri mahakamani au kwenye baraza.

(3) Wakala unaweza, baada ya kutoa taarifa kwa muda unaoridhisha ya kusudio lake la kuchukua hatua hizo, kuelekeza taasisi, idara, mamlaka, mtu au watu, kutekeleza, ndani ya muda utakaopangwa na kwa namna kama utakavyoelekeza, kazi yoyote au nyingine iliyowekwa na au chini ya Sheria hii au Sheria nyingine yoyote kuhusiana na usimamizi na utekelezaji wa Sheria.

(4) Endapo itatokea kushindwa kutekeleza maelekezo hayo, Wakala unaweza kufanya au kusababisha kufanyika kazi zinazotakiwa na gharama zitakazotumika zitarudishwa na Wakala kutoka kwenye taasisi, idara, mamlaka, mtu au watu hao kwa njia ya madai.

Baraza la
Usimamizi
wa Maafa
Tanzania

7.-(1) Kutakuwa na Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania.

(2) Baraza litaundwa na wajumbe wafuatao-

- (a) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Usimamizi wa maafa ambaye atakuwa Mwenyekiti;

- (b) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye atakuwa Makamu wa Mwenyekiti;
- (c) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (d) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya mamlaka ya tawala za mikoa na Serikali za Mitaa;
- (e) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya fedha;
- (f) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya afya na ustawi wa jamii;
- (g) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya mawasiliano;
- (h) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Mazingira;
- (i) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Kilimo;
- (j) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya Maji;
- (k) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi;
- (l) Katibu Mkuu Wizara yenye dhamana ya mambo ya jiolojia; na
- (m)Mkurugenzi Mkuu WA Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania.

(3) Mkurugenzi Mkuu wa Wakala atakuwa Katibu wa Baraza.

(4) Baraza linaweza kumualika mtu yeyote wakati wa Mkutano wake kadiri litakavyoona inafaa.

(5) Masharti ya Jedwali la Sheria hii yatahusu shughuli za Baraza na mambo mengine yanayohusiana nalo.

Kazi za
Baraza

8.-(1) Baraza litasimamia shughuli za Wakala.

(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Baraza litakuwa na jukumu la-

- (a) kuhakikisha kwamba upunguzaji wa athari za maafa unajumuishwa katika taasisi stahiki za Serikali, sera za maendeleo, mikakati, program na mipango katika ngazi ya taifa, mkoa na mtaa;
- (b) kutoa msaada katika utafutaji wa rasilimali ili kuwa na ufanisi katika kupunguza athari za maafa;
- (c) kuhamasisha uandaaji wa mikakati ya kitaifaya upashaji wa taarifa na maarifa na uanzishaji wa mitandao ya wadau ya Usimamizi wa athari za maafa;
- (d) kupitia na kuboresha sera za Usimamizi wa maafa; na

(e) kumshauri Waziri kuhusiana na Usimamizi wa maafa na mambo yote yanayohusiana.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA WAKALA

Mkurugenzi
Mkuu

9.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa husika.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuhuli wa Wakala na atawajibika kwa Baraza.

Mamlaka ya
Mkurugenzi
Mkuu

10.-(1) Mkurugenzi Mkuu, anaweza, wakati wa hali ya hatari na baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Baraza kutoa maelekezo au amri ambayo ni muhimu katika kushughulikia jambo husika.

(2) Mkurugenzi Mkuu baada ya kushauriana na Mwenyekiti-

(a) atamfahamisha Waziri kuhusu hatua za dharura zilizochukuliwa ili kukabili hali iliyotokea;

(b) atashauri atashauri kifanyike kikao cha dharura cha Baraza ili kutoa maamuzi kuhusu hali iliyotokea.

Kurugenzi na
watumishi
wa Wakala

11.-(1) Wakala kwa idhini ya Mamlaka husika, unaweza kuanzisha kurugenzi, vitengo kwa kwa kuzingatia umuhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Wakala.

Sura ya 298

(2) Wakala, kwa idhini ya Baraza na kwa mujibu wa Sheira ya Utumishi wa Umma, utateua au kuajiri idadi ya maofisa kadiri itakavyolazimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi chini ya sheria hii.

Kitabu cha
orodha na
vifaa

12.-(1) Mkurugenzi Mkuu atanzisha na kutunza kitabu cha orodha ya vitu kwa ajili ya misaada ya kibinadamu na miundombinu muhimukwa ajili ya shughuli za operesheni za maafa.

(2) Kitabu au orodha iliyoandaliwa na Wakala itakuwa ni nyaraka rasmi ya kiofisi kwa matumizi ya Wakala, na Wakala unaweza ukashirikisha taarifa zilizomo katika kitabu au orodha kwa mtu mwingine yeyote, idara au taasisi kama atakavyoona inafaa.

(3) “Miundombinu muhimu” kama ilivyotumika katika kifungu kidogo cha (1), maana yake ni michakato, mifumo, nyenzo, teknolojia, mitandao, rasilimali na huduma muhimu za afya, usalama, ulinzi au ustawi wa kiuchumi na ufanisi wa utekelezaji wa kazi za Serikali au jamii.

Kamati ya
Mkoa ya
Usimamizi
wa Maafa.
Sura ya 97

13.-(1) Sekretarieti ya Mkoa iliyoanishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, itakuwa Kamati ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa katika mamlaka ya mipaka yake.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) na kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Tawala za Mikoa, Kamati ya Mkoa pamoja na Wajumbe wa Sekretarieti ya Mkoa ikiwajumuisha wajumbe wafuatao waliochaguliwa na Katibu Tawala wa Mkoa-

- (a) mratibu wa Usimamizi wa maafa wa mkoa ,
- (b) mwakilishi kutoka jumuiya ya asasi zisizo za serikali za mkoa;
- (c) wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi ndani ya mkoa;
- (d) mwakilishi wa Mkoa wa Chama cha Msalaba Mwekundu na asasi nyingine za kibinadamu na za kujitolela;
- (e) wawakilishi watatu kutoka taasisi za dini; na
- (f) watu wawili mashuhuri.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), kamati ya Mkoa inaweza, muwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa kamati kushiriki katika kikao cha maamuzi kamati.

(4) Mratibu wa Usimamizi wa Maafa wa Mkoa, kwa madhumuni ya kifungu hiki, atakuwa Katibu wa Kamati ya Mkoa.

Kazi za
Kamati ya
Mkoa

14. Kazi za Kamati ya Mkoa zitakuwa-

- (a) kumshauri Mkuu wa Mkoa kuhusu masuala ya Usimamizi wa maafa na shughuli zinazofanywa mkoani na mambo mengine yoyote yatakayoletwa na Mkuu ya Mkoa;
- (b) kuangalia na kuratibu shughuli za upunguzaji na Usimamizi wa athari za maafa na shughuli za dharura miongoni mwa taasisi za kissekta za Serikali, Serikali za mitaa, jamii na wadau wengine wanaojihusisha katika upunguzaji na Usimamizi wa athari za maafa;

- (c) kutafuta rasilimali kwa ajili ya Usimamizi wa maafa katika mkoa yao;
- (d) kufungamanisha mfumo wa tahadhari ya awali katika Mkoa na kuwezesha uanzishaji wa mfumo wa takwimu na taarifa za maafa za mkoa kwa kushirikiana na Wakala; na
- (e) kuratibu mipango ya Wilaya ya Usimamizi wa maafa iliyowasilishwa na Kamati ya Wilaya.

Kamati za
Wilaya

15.-(1) Kamati ya Usimamizi wa Halmashauri iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) na Sheria ya Serikali ya Mtaa (Mamlaka za Wilaya) kwa madhumuni ya Sheria hii, zitakuwa Kamati za Wilaya za Usimamizi wa Maafa katika mamlaka ya Wilaya husika.

(2) Bila ya kuathiri kifungu akidogo cha (1) na masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) na Sheria ya Serikali ya Mtaa (Mamlaka za Wilaya) kuhusu kuanzishwa wa Usimamizi wa Halmashauri, Kamati za Wilaya zitajumuisha wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Halmashauri pamoja na wajumbe walioteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji wafuatao-

- (a) mratibu wa Usimamizi wa maafa wa Wilaya;
- (b) wawakilishi wawili wa sekta binafsi ndani ya Wilaya;
- (c) wawakilishi katoka jumuiya ya Wilaya ya Asasi zisizo za Serikali;
- (d) watu wawili mashuhuri;
- (e) mwakilishi wa Wilaya wa Chama cha Msalaba Mwekundu na taasisi nyingine za kibinadamu na za kujitolea;
- (f) wawakilishi watatu wa taasisi za dini;

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa ataona ni lazima, kumwalika kumwita mtu yeyote ambaye si mjumbe wa kamati kuhudhuria majadiliano ya kamati.

(4) Mratibu wa Usimamizi wa maafa wa Wilaya, kwa madhumuni ya kifungu hiki, atakuwa katibu wa kamati wa Wilaya;

Makujumu
ya Kamati za
Wilaya

16. Majukumu ya Kamati za Wilaya zitakuwa-

- (a) kumshauri Mkuu wa Wilaya kuhusu masuala ya Usimamizi wa maafa na kufanya shughuli zinazofanyika ndani ya wilaya na mambo mengine yaliyoelekezwa na Mkuu wa Wilaya;
- (b) kuangalia na kuratibu athari za Usimamizi wa maafa na shughuli za dharura katika ngazi ya wilaya;

(c) kutafuta rasilimali zinazohusiana na Usimamizi wa maafa.

Uwezo wa kamati za Mkoa na Wilaya

17. Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mkoa na Wilaya kwa kushirikiana na Wakala, zitakuwa na uwezo wa-

- (a) kuelekeza taasisi zote katika Mkoa na Wiaya kujiandaa, kuzuia au kupunguza maafa;
- (b) kuamuru watu kuondoka katika maeneo hatarishi au yaliyoathirika na maafa na kuwahamishia maeneo mengine;
- (c) kumuomba mtu yeyote au asasi ndani ya mkoa au wilaya kutoa usafiri, jengo lolote, vifaa, bidhaa muhimu na vitu vingine kwa ajili ya kusaidia jitihada za Usimamizi wa maafa katika wilaya;
- (d) kuanzisha kamati ndogo ndogo kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi zake;
- (e) kufanya jambo lolote ambalo ni la lazima kufanywa kwa ajili utekelezaji wa kazi zake chini ya sheria hii kutegemeana na sera, mipango na taratibu;

Kamati za kata

18.(1) Vikundi vya usimamizi vya Kata vinavyoundwa chini ya sheria ya Serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya) kwa madhumuni ya sheria hii, zitakuwa kamati za Usimamizi wa maafa za Kata kutoka maeneo ya mamlaka zao.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), na masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) kuhusu uundaji wa vikundi vya usimamizi vya kata, kamati za Kata kwa kujumuisha wajumbe wa vikundi vya usimamizi za kata, zitajumuisha wajumbe wafuatao ambao wameteuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushauriana na Afisa Mtendaji wa Kata.

- (a) wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi ndani ya Kata;
- (b) wawakilishi wa taasisi za kijamii ndani ya Kata;
- (c) watu wawili mashuhuri;
- (d) mwakilishi kutoka chama cha msalaba mwekundu na taasisi nyingine za kibinadamu na za kujitolea; na
- (e) wawakilishi watatu kutoka taasisi za dini.

(3) Afisa Mtendaji wa Kata anaweza, iwapo ataona kuna ulazima, kumjumuisha mtu yeyote ndani ya kata husika ambaye si mjumbe wa Kamati kuhudhuria kikao cha Kamati.

(4) Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa Kata, anaweza kumteua afisa kilimo yeyote wa kata kuwa Katibu wa kamati ya Kata kwa madhumuni ya kifungu hiki.

Kazi za
Kamati za
Kata

19. Kazi za Kamati za Kata zitakuwa ni:

- (a) kusimamia na kuratibu usimamizi wa athari za maafa na operesheni ya shughuli za dharura katika ngazi ya Kata;
- (b) kutafuta rasilimali kwa ajili Usimamizi wa maafa;
- (c) kusaidia utekelezaji wa mipango ya Usimamizi wa maafa ya kata;
- (d) kuwa na muitikio katika namna iliyo iliyoratibiwa, katika ngazi ya kata.

Kamati za
Vijiji

20.-(1) Kamati ya Maendeleo ya kijiji iliyoanzishwa chini ya sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) kwa madhumuni ya sheria hii, itakuwa Kamati za Usimamizi wa Maafa ya Kijiji katika maeneo ya mamlaka yake.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) na masharti ya sheria ya Serikari za Mitaa(Mamlaka za Wilaya) kuhusu uundaji wa Kamati za Maendeleo za Vijiji, kamati ya Kijiji kwa kujumuisha wajumbe wa Kamati ya maendeleo ya Kijiji. itajumuisha wajumbe wafuatao walioteuliwa na Mkurugezi wa Halmashauri kwa kushauriana na Afisa Mtendaji wa Kijiji:

- (a) wawakilishi wawili wa sekta binafsi zilizopo katika kijiji;
- (b) mwakilishi wa jumuiya za asasi zisizo za Serikali zilizopo katika kijiji;
- (c) watu wawili mashuhuri;
- (d) mwakilishi kutoka chama cha msalaba mwekundu na au hilal nyekundu na taasisi za kibinaadamu na za kujitolea; na
- (e) wawakilishi watatu kutoka taasisi za dini ndani ya Kijiji

(3) Bila ya kujali masharti ya kufungu kidogo (2), Afisa Mtendaji wa kijiji pale anapoona ni lazima, anaweza kumwita mtu yeyote kutoka ndani ya kijiji husika ambaye si mjumbe wa kamati kushiriki kikao cha Kamati.

(4) Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushuriana na Afisa Mtendaji wa Kijiji atamteua afisa yeyote ndani ya kijiji kuwa Katibu wa Kamati ya Kijiji kwa madhumuni ya kifungu hiki.

Kazi za
Kamati za
vijiji

21.-(1) Kazi za Kamati ya Kijiji zitakuwa ni-

- (a) kusimamia na kuratibu Usimamizi wa athari za maafa na operesheni ya shughuli za dharura katika ngazi ya kijiji;
- (b) kuchukua nafasi ya chombo cha taarifa kuhusiana na utoaji tahadhari ya awali katika kijiji;
- (c) kutafuta rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za maafa;
- (d) kutekeleza mipango ya utoaji taarifa na kujenga uelewa katika vijiji; na
- (e) kukabili dharura katika utaratibu ulioratibiwa katika ngazi ya kijiji.

(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, kamati ya kijiji kadiri itakavyowezezana itatumia sheria za kimila, taratibu za kimila na mbinu za kiasili za tahadhari na mawasiliano.

Utoaji
taarifa za
usimamizi
wa maafa

22.- (1) Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mkoa na Kamati za Usimamizi wa Maafa za Wilaya, katika kila robo mwaka au kwa kadiri zitakavyoelekezwa, zitaanda na kuwasilisha katika Kamati za Usalama husika taarifa za kina kuhusu utekelezaji wa upunguzaji wa athari za maafa na usimamizi wake katika mamlaka zake husika.

(2) Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazo ainisha namna ya uandaaji na uwasilishwaji wa taarifa za utekelezaji wa upunguzaji wa athari za maafa na usimamizi wake katika ngazi ya Kamati za Usimaizi wa Maafa za vijiji na kata.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maneno “Kamati za Usalama” maana yake ni Kamati za Usalama za Mikoa na Kamati za Usalama za Wilaya zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa.

Sura ya 61.

Miongozo ya
utendaji kazi
wa Kamati

23.-(1) Waziri anaweza kutengeneza miongozo kwa ajili ya usimamizi mzuri wa kamati za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji.

- (2) Miongozo iliyotengenezwa chini ya kifungu hiki itaelezea-
 - (a) utayarishaji wa mipango katika ngazi mbalimbali za Kamati;
 - (b) njia za mawasiliano na usambazaji wa taarifa zinazohusu upunguzaji na Usimamizi wa athari za maafa ;
 - (c) usambazaji wa taarifa zinazohusu tahadhari ya awali;
 - (d) uendeshaji wa shughuli za Kamati.

(3) Waziri anaweza kutunga miongozo maalum kwa kamati mojawapo ya zilizoainishwa.

Udhibiti wa
masuala ya
kamati za
maafa

24. Kamati za Mkoa, Wilaya, Kata na vijiji zitadhibiti mambo yao katika mamlaka zao husika.

**SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA KULINDA RAIA**

Utaratibu wa
kulinda raia

25.-(1) Wakala utaweka taratibu za kulinda raia kwa mamlaka za serikali za mitaa, taasisi za Serikali, na asasi za Sekta mbalimbali zinazojihusisha na Usimamizi wa maafa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) wakala utachukua hatua ambazo ni za lazima ili kuendeleza programu za kujenga uwezo kwa Kamati za Mkoa na Wilaya, taasisi za serikali na taasisi za sekta mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma za lazima na za taratibu za kufuatwa katika kukabili maafa na kurejesha hali.

(3) “Ulinzi wa raia” kama ilivyotumika katika kifungu hiki, ina maana ya juhudi za pamoja za vitengo tofauti vya dharura katika kuandaa jamii kujilinda na majanga yanayoelekea kusababisha maafa.

Wajibu wa
jumla

26. Kila mtu ana wajibu wa -

- (a) kuweka mpangilio wa ustawi wa jamii na kutunza amani na mapatano;
- (b) kuwa na mienendo ambayo itapunguza athari za maafa; na
- (c) onesha utayari na kuridhia kushiriki katika shughuhuli za Usimamizi wa maafa.

**SEHEMU YA TANO
OPERESHENI WAKATI WA MAAFA NA HALI YA HATARI**

Kutangaza
maafa

27.-(1) Endapo wakala utakaporidhika kwamba hali ya dharura inayopelekea kuwepo kwa maafa katika eneo, utahuisha Mpango wa Taifa wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa kutumika katika eneo hilo kwa kipindi cha miezi mitatu.

(2) Endapo Mpango wa Taifa wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa umehuishwa katika eneo, Waziri atatoa amri kwenye Gazeti la Serikali, kuweka utaratibu wa shughuli ambazo zitatumika katika eneo hilo.

(c) Hali ya Hatari

Hali ya dharura inayopelekea kusababisha maafa

28.-(1) Endapo hali ya dharura inapongezeka na kupelekea kusababisha maafa ambayo kwa uhalisia wake na ukubwa wake itahitajika kuchukua hatua za kipekee, Baraza litapendekeza kwa Waziri kwamba hali ya hatari itangazwe katika eneo la maafa au kwa Tanzania Bara yote.

(2) Endapo Waziri ataridhika kwamba hali ya maafa inalazimu kutolewa kwa tamko la hali ya hatari, Waziri, kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika kifungu cha 4 cha sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hatari atamtaarifu Rais juu ya matukio mbalimbali yanayolazimu au kupelekea kutolewa kwa tamko la hali ya hatari katika eneo husika.

(3) Tamko la hali ya Hatari litajumuisha na kueleza hatua za haraka ambazo zitakazochukuliwa ikijumuisha-

- (a) kuwahamisha au kuwaondoa watu na mali zao;
- (b) kutumia msaada wa Jeshi;
- (c) kupata msaada wa kimataifa;
- (d) hatua nyingine kama itakavyokuwa lazima kulingana na hali halisi ya mazingira.

SEHEMU YA SITA

MPANGO WA TAIFA USIMAMIZI WA MAAFA

Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa

29.-(1) Wakala kwa kibali cha Waziri, utatayarisha na kutunza mpango wa Taifa wa Usimamizi wa maafa.

(2) Mpango wa Taifa wa usimamizi wa maafa utauunganishwa katika mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka na utakuwa unahuishwa na kutengenezwa kama ni lazima.

(3) Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa maafa utawezesha kuingiza masuala ya upunguzaji wa athari za maafa na katika mipango ya maendeleo na kisekta na itatumiwa na Wakala, Kamati za Mkoa na Wilaya na Serikali na asasi mbalimbali katika Usimamizi wa maafa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3) Kila Wakala, Kamati za Mkoa na Wilaya, Serikali na asasi mbalimbali za kisekta zitaandaa na kuwasilisha taarifa ya mwaka kwenye Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa kwa majadiliano na kupeana uzoefu.

(5) Waziri, kwa kanuni atatoa tamko kwa mambo ambayo yatajumuishwa katika mpango wa Taifa wa Usimamizi wa maafa.

**SEHEMU YA SABA
MFUKO WA USIMAMIZI WA MAAFA**

Mfuko wa
Taifa wa
Usimamizi
wa maafa

30.-(1) Kutakuwa na Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa maafa.

(2) Vyanzo vya fedha vya Mfuko vitakuwa-

- (a) kiasi cha fedha ambacho kitadhiniswa na Bunge kwa madhumuni ya Usimamizi wa maafa;
- (b) mchango wa hiari kwa Mfuko kutoka kwa mtu yeyote au taasisi;
- (c) fedha yoyote ambayo imetolewa kwa njia kya msaada au mkopo kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano.
- (d) fedha yoyote iliyopatikana kwa njaa mauzo ya vitu vilivyotolewa kama msaada; na
- (e) kutokana na harambee;

(3) Mfuko utasimamiwa na Wakala na Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye Afisa Masuhuli.

(4) Fedhda zitatumika kwa-

- (a) kutoa bidhaa muhimu na misaada mingine kwa waathirika wa maafa yoyote, janga au dharura; na
- (b) kuzuia, kupunguza athari, kujiandaa, kukabili na kurudisha hali katika maafa na shughuli nyingine zinazohusu usimamizi wa maafa.

Usimamizi
wa
makusanyo
na misaada

31.-(1) Wakala unaweza kuendesha mchango maalum au wa jumla kwa jamii kuchangia vitu au fedha kwa madhumuni ya kuokoa maisha, mali, kupunguza uharibifu au kurejesha mfumo maisha ya jamii iliyoathirika na maafa.

(2) Endapo kuna mantiki kwa ombi la wakala, mtu yeyote au taasisi inayokusanya vitu au fedha, itatakiwa kuwasilisha taarifa kwa wakala, kuelezea vitu vilivyokusanywa na fedha ambayo vitu hivyo au fedha ziligawiwa kwa jamii iliyoathirika na maafa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), misaada kwa jamii iliyoathirika na maafa itapelekwa moja kwa moja kwa jamii husika au kupitia kamati za Mkoa au Wilaya, Wakala au viongozi wa Kitaifa.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya
fedha

- 32.**-(1) Vyanzo vya fedha za Wakala vitajumuisha-
- (a) fedha kama zitakavyotengwa na Bunge ;
 - (b) fedha zozote au rasilimali ambazo zinaweza kuwekwa au kupatikana kutoka kwenye vyanzo vingine;
 - (c) ada zilizowekwa na malipo mengineyanayokusanywa kutoka katika huduma zilizotolewa.
 - (d) zawadi, mikopo na michango;
 - (e) fedha zinazopatikana kutokana na mauzo ya rasilimali za wakala; na
 - (f) fedha nyingine yoyote, iliyokopwa, kupokelewa na, au iliyopatikana kwa ajili ya kazi za Wakala.

(2) Ada na malipo yanayolipwa chini ya Sheria hii yataainishwa kwenye kanuni.

Taarifa ya
mwaka na
mahesabu

33.-(1) Katika sheria “mwaka wa fedha” maana yake ni mwaka wa fedha wa Serikali.

(2) Mkurugenzi Mkuu, mwishoni mwa kila “mwaka wa fedha” atatayarisha taarifa ya utekelezaji ya mwakakuhusu shughuli zilizotekelezwa na wakala na kuwasilishwa kwa Waziri baada ya kuidhinishwa na Bodi.

(3) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba, taarifa ya fedha ya mwaka inaandaliwa na kukaguliwa ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha.

- (4) Taarifa ya fedha itajumuisha-
- (a) taarifa ya utendaji wa fedha;
 - (b) taarifa ya hali ya fedha;
 - (c) taarifa ya mtiririko wa fedha;
 - (d) taarifa ya mabadiliko ya mtaji; na
 - (e) tangazo la taarifa ya fedha.

Uwasilishaji
wa tarifa ya
mwaka

34.-(1) Mkurugenzi Mkuu atawasilisha kwa Waziri taarifa ya fedha zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha wa kila mwaka.

(2) Mkurugenzi Mkuu atatarisha na kuwasilisha kwenye baraza makadirio ya mapato na matumizi ya wakala miezi mitatu kabla ya mwisho wa mwaka unaoisha.

(3) Hakuna matumizi ya fedha za Wakala yatakayofanywa kutokana na fedha za Wakala isipokuwa kama yameidhinishwa na Mkurugenzi katika mwaka huo wa fedha.

Usimamizi
na udhibiti
wa fedha

35.-(1) Wakala utatunza vitabu vya mahesabu na kuweka kumbukumbu za shughuli zake kulingana na viwango vya mahesabu ya Kitaifa.

(2) Wakala atasababisha kutayarishwa na kutunzwa vizuri vitabu vya mahesabu na kumbukumbu kufuatana na-

- (a) rasilimali na madeni;
- (b) mapato na matumizi ya fedha na miamala mingine ya fedha;
- (c) taarifa ya hali ya fedha na taarifa ya utendaji wa fedha itakaotayarishwa kila mwaka wa fedha;

(3) Fedha na rasilimali za Wakala zitatumika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo ya Sheria hii.

(4) Matumizi ya Wakala yatawajibika kusimamiwa na kufanyiwa mapitio.

Bajeti ya
mwaka na ya
nyongeza

36.-(1) Baraza litaidhinisha bajeti ya mwaka ya kiasi kinachotarajiwa kupokelewa na kulipwa kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha, si chini ya mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wowote.

(2) Endapo katika mwaka wowote wa fedha, Wakala inataka kufanya malipo yoyote ambayo hayakutolewa au kiasi chochote kinachozidi kiasi ambacho kiliwekwa katika bajeti ya mwaka huo, Baraza itaidhinisha bajeti ya nyongeza inayoelezea malipo hayo.

(3) Bajeti ya Mwaka na kila bajeti ya nyongeza itakuwa katika fomu na itajumuisha maelezo kama yatakavyotakiwa na sheria.

Kanuni za
uendeshaji

37. Wakala-

- (a) utafungua na kuendesha vitabu vyote vya mahesabu, leja, jarada na vitabu vingine vya mahesabu kufuatana na kitabu cha mwongozo wa mahesabu;

(b) utapitia na kubadili nyaraka zake kwa ajili ya kuwezesha uwekaji mzuri wa vitabu vya mahesabu kama itakavyoelekezwa na mamlaka husika.

(2) Fedha zote zilizopokelewa zitawekwa katika akaunti ya mapato na malipo yatafanywa kutoka katika akaunti ya matumizi

(3) Hakuna matumizi yoyote yatakayofanyika kutoka katika fedha za Wakala, vinginevyo matumizi hayo yawe ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Baraza.

Uwezo wa kuwekeza

38. Wakala kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha, unaweza kuwekeza fedha yoyote katika namna ambayo itaona inafaa.

SEHEMU YA TISA MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

39. Mtu ambaye-

(a) anachelewesha au kumzuia afisa yeyote kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii.

(b) anakataa kutoa ushirikiano unaofaa kwa afisa yeyote kama atakavyoombwa na afisa kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake chini ya sheria hii.

(c) anatoa taarifa za uongo au za kupotosha kwa makusudi wakati akijibu maswali ya afisa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya fedha zisizopungua shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote viwili.

anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopzidi shilingi milioni moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Makosa yanayosababi shwa na mashirika

40. Endapo kosa linapokuwa limetendwa au watu au kampuni, mtu yeyote ambaye wakati wa muda wa kutenda kosa alikuwa kwenye usimamizi wa shughuli za kundi la watu au kampuni hodhi, litachulikuwa kuwa kosa limetendwa.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI YA MCHANGANYIKO

Jukwaa la
Menejimenti
wa Maafa

41.-(1) Kutokuwa na Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa ambalo litatoa nafasi ya wadau kukutana na kujadili mikakati inayohusu Usimamizi wa maafa na kuishauri Serikali kikamilifu.

(2) Jukwaa litaundwa na-

- (a) Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa ni mwenyekiti;
- (b) Wakuu wa Idara yenye dhamana na usimamizi wa maafa kutoka:
 - (i) Wizara yenye dhamana na Kilimo na Chakula;
 - (ii) Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi;
 - (iii) Wizara yenye dhamana na Fedha;
 - (iv) Wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa;
 - (v) Wizara yenye dhamana na Afya na Ustawi wa Jamii;
 - (vi) Wizara yenye dhamana na Mazingira
 - (vii) Wizara yenye dhamana na Nishati na Madini;
 - (viii) Wizara yenye dhamana na Mambo ya Nje;
 - (ix) Wizara yenye dhamana na Mawasiliano na Habari;
 - (x) Wizara yenye dhamana na Ardhi na Nyumba;
 - (xi) Wizara yenye dhamana na Usafiri;
 - (xii) Wizara yenye dhamana na Wanawake, Jinsia na Watoto;
 - (xiii) Wizara yenye dhamana na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;
 - (xiv) Wizara yenye dhamana na Maliasili na Utalii; na
 - (xv) Wizara yenye dhamana na mambo yanayohusiana na nguvu za atomu;
- (c) Wakuu wa taasisi zifuatazo:
 - (i) Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania;
 - (ii) Kikosi cha zimamoto;
 - (iii) wakala wa taifa wa akiba ya chakula;
 - (iv) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
 - (v) Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania
 - (vi) Ofisi ya Upimaji wa Jeologia Tanzania;
 - (vii) Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania;
- (d) mwakilishi wa wakala wa Hali ya hewa;
- (e) watu wane wanaowakilisha taasisi za elimu ya zinazotambulika;
- (f) mwakilishi wa jeshi la wananchi Tanzania;

- (g) mwakilishi wa taasisi yenye dhamana na Mipango ya Taifa;
- (h) wawakilishi watatu walioko chini ya mwamvuli wa asasi za kiraia;
- (i) Mwakilishi wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania;
- (j) wawakilishi wawili walioko chini ya mwamvuli wa mashirika ya kimataifa;
- (k) mwakilishi wa Sekta Binafsi inayoshughulikia masuala ya maafa;
- (l) mwakilishi wa mashirika yanayoshughulika na utoaji wa huduma za kibinadamu;
- (m)mwakilishi wa watoa huduma ya habari;
- (n) wawakilishi watatu kutoka taasisi za dini;
- (3) Jukwaa linaweza kumualika mtu mwingine yeyote kama itakuwa ni lazima.

(4) Jukwaa litakutana angalau mara mbili kwa mwaka lakini linaweza kukutana wakati mwingine wowote kama kutakuwa na suala ambalo linahitaji kujadiliwa haraka.

(5) Jukwaa litaweka taratibu za kuendesha vikao vyake.

(6) Jukwaa laweza kuunda kamati ambazo wajumbe wake watateuliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Jukwaa.

Kinga dhidi
ya mashtaka

42.-(1) Mwajiriwa yeyote wa Wakala hatashtakiwa binafsi kwa jambo lolote alilolitenda au kuacha kutenda kwa nia njema akitekeleza au kuchukuliwa kutotekeleza kazi yoyote akiwa kama mwajiriwa wa wakala.

(2) Wakala itamlipa na kumrudishia kwa kiwango cha namna kama itakavyoelezwa mtu anayejitolea na mtu mwingine aliyeshughulika na usimamizi wa maafa gharama za msingi alizolingia ikiwa ni matokeo ya-

- (a) kutekeleza mwikitio wa kutoa huduma za maafa kwa mujibu wa sheria hii;
- (b) kupatikana kwa ajali ya maafa, ardhi , yoyote au vituo.

Kanuni

43. Waziri atatunga Kanuni kuhusu jambo lolote litakalohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji au wa kuipa nguvu utekelezaji wa sheria hii.

Kufuta na
kubakiza
Sura 242

44.-(1) Sheria ya Uratibu wa Misaada ya Maafa inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa huko kwa sheria, kanuni, amri, au matangazo ya serikali, yaliyotolewa chini ya Sheria ya Uratibu wa Maafa na ambayo bado yananguvu mara kabla ya Sheria hii kuanza kutumika kwa Sheria hii, yataendelea kuwa na nguvu kana kwamba yametolewa chini ya Sheria hii.

JEDWALI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(5))

UTARATIBU WA MIKUTANO YA BARAZA NA MAMBO MENGINE

Mikutano ya
Baraza

1.-(1) Baraza litakutana kwa kuendesha shughuli zake katika muda na sehemu itakayoamuliwa na Baraza.

(2) Mikutano ya kawaida ya Baraza itafanyika mara moja kwa kila miezi mitatu.

(3) Mwenyekiti au ikiwa kama hayupo Makamu Mwenyekiti anaweza katika wakati wowote kuitisha kikao cha dharura cha Baraza, baada ya kupokea ombi la kimaandishi kutoka kwa wajumbe wengi wa Baraza.

(4) Mwenyekiti au kama hayupo, Makamu mwenyekiti ataongoza mikutano ya Baraza.

(5) Mwenyekiti au kama hayupo, Makamu Mwenyekiti anaweza kumwalika mtu mwingine ambaye si mjumbe kuhudhuria mkutano wowote wa kamati isipokuwa kupiga kura.

Akidi

2. Akidi ya mkutano wowote wa Baraza itakuwa ni nusu ya wajumbe wa Baraza.

Uamuzi wa
Baraza

3.-(1) Swala linaloletwa katika Baraza litaamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria wakati wa upigaji kura na kama kura zitakuwa sawa, mtu anayeongoza kikao atakuwa na kura ya uamuzi.

(2) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (1), uamuzi wa Baraza unaweza kufanywa bila ya Mkutano kwa njia ya mzunguko wa hati husika miongoni mwa wajumbe na mwelekeo wa maandishi wa maoni ya wengi ya wajumbe ndio utakaokuwa uamuzi wa wengi.

Kumbukumbu za kikao

4.-(1) Baraza litahakikisha kumbukumbu za mkutano zinachukuliwa na kutunzwa na kumbukumbu zitatumwa au kurekebisha na kuidhinishwa katika mkutano wa Baraza na kusainiwa na mtu anayeongoza kikao.

(2) Kumbukumbu zitasainiwa na mtu anayeongoza kikao cha Baraza kwa uthibitisho wa kutokuwepo kwa makosa, zitachukuliwa kuwa kumbukumbu sahihi za kikao.

Kutokuhudhuria hakutaharamisha kikao

5. Uhalali wa kikao au jambo lolote la Baraza halitaathiriwa kwa sababu ya kutokuwepo kwa mmoja kati ya wajumbe au kosa lolote la uteuzi wa mmoja wao.

Amri, maelekezo, matangazo au hati

6. Amri, maelekezo, matangazo au hati zilizoandaliwa au kutolewa kwa niaba ya Baraza zitasainiwa na-

(a) Mwenyekiti; au

(b) Mkurugenzi Mkuu au Ofisa mwingine yeyote wa Wakala aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu.

Lakili ya Baraza

7. Lakili ya Baraza na haitawekwa kwenye hati yoyote isipokuwa mbele ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mkurugenzi Mkuu.

Baraza kuweka taratibu zake

8. Kwa mujibu wa masharti ya Jedwali hili, Baraza linaweza kuweka namna ya kuendesha taratibu zake.

Imepitishwa na Bunge tarehe 26 Machi, 2015

THOMAS D. KASHILILAH
Katibu wa Bunge